

THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY



KIBWETA CHA MWALIMU NYERERE “KITUO CHA UONGOZI NA MAADILI”

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UONGOZI, MAADILI NA UTAWALA
BORA KATIKA “KIBWETA CHA MWALIMU NYERERE” KILICHOPO CHUO CHA
KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE
MAFUNZO YATAANZA TAREHE 16 OKTOBA, 2017**

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kupitia *Kibweta cha Mwalimu Nyerere cha Uongozi na Maadili*, kinapenda kuwatangazia wadau wote kwamba awamu nyingine ya mafunzo ya Uongozi, Maadili na Utawala Bora imepangwa kuanza tarehe 16 oktoba, 2017 katika Kampasi ya Kivukoni – Kigamboni, Dar es Salaam.

MALENGO YA MAFUNZO:

- Kujenga uelewa wa nadharia ya maadili nautawala bora na misingi ya utumiaji wa uelewa huo katika maeneo ya kazi.
- Kuboresha weledi wa viongozi katika kutatua migogoro na kufanya makubaliano ya kidiplomasia sehemu za kazi.
- Kujenga uwezo wa kupanga mipango mikakati, kufanya uongozi wa miradi na ujasiriamali endelevu, na
- Kuendeleza uwezo wa kufanya maamuzi kama viongozi na kupanua kiwango cha uelewa wa maadili na utawala bora.

WALENGWA:

Viongozi watarajiwa na waliopo kazini katika ngazi za kufanya maamuzi. Hivyo, Viongozi mbalimbali katika Wizara, Taasisi, Vyama mbalimbali, Mashirika ya Umma na binafsi wanaombwa kujiunga na mafunzo haya ya Uongozi na Maadili ili kuinua uelewa wao katika nyanja hii muhimu kwao binafsi na kwa taasisi/idara wanazozisimamia.

MUDA WA MASOMO:

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa miezi mitatu, ambapo wiki mbili za mwanzo wa mafunzo zitatumika kwa masomo ya darasani (nadharia) na miezi miwili na nusu inayofuatia itakuwa ni mafunzo kwa njia ya vitendo nje ya Chuo, ambapo washiriki watarejea kwenye maeneo yao ya kazi na kuendelea na kazi zao za kawaida kwa sharti kwamba katika kipindi hicho watasimamiwa na wakufunzi wao kutoka Kibweta cha Mwalimu Nyerere pamoja na kufanyiwa tathmini. Aidha mafunzo yatatolewa kuanzia saa tatu kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni (03.00 – 10.00) katika siku za kazi (jumatatu hadi ijumaa).

ADA ya mafunzo kwa awamu ya kwanza ya miezi mitatu ni Tshs. 1,200,000/= (shilingi Milioni moja na laki mbili tu). Gharama hii inajumuisha huduma zitakazotolewa wakati wa mafunzo ikiwa ni pamoja na kifungua kinywa. Usafiri na malazi ni ya kujitegemea.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **13 Oktoba, 2017.**

‘Maadili ndiyo moyo wa Uongozi’.

Maombi yatumwe kwa:

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,
DAR ES SALAAM

Simu: +255 22 2820041/2820047 au 0756270610
Barua pepe: rector@mnma.ac.tz
Tovuti: www.mnma.ac.tz